**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**

**Kumb. Na. HW/MUF/S.50/19VOL.XI/125** **25 Novemba, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (AJIRA YA MUDA)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mufindi anawatangazia Wananchi wa kata ya Mbalamaziwa wenye sifa na nia ya kufanya kazi ajira ya muda katika Halmashauri ya Wilaya Mufindi kuomba nafasi ya kazi ya Waendesha mtambo wa kuzalishia kokoto, wagonga mawe, wabeba mawe na mlinzi kwa mchanganuo ufuatao;

## 1.0 WAENDESHA MTAMBO (NAFASI 2)

### 1.1 KAZI NA MAJUKUMU.

i. Kuendesha Mtambo wa kuzalishia kokoto.
ii. Kufanya marekebisho na maboresho madogo madogo ya mtambo
iii. Kutoa taarifa ya uendeshaji wa mtambo kwa msimamizi wa mradi
iv. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

#### 1.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe amehitimu kidato cha nne, Leseni ya Udereva Class 'G' Mtiifu na mwaminifu,awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa na awe Mkazi wa Kata ya Mbalamaziwa.

#### 1.1.2 Malipo

Malipo yatakuwa Tshs.10,000/= kwa siku na malipo hayo yatafanyika mwisho wa mwezi.

## 2.0 WAPASUA MAWE (NAFASI 4)

### 2.1 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kupasua mawe na kuhakikisha yanakuwa katika ukubwa unaofaa kabla ya kupeleka kwenye mtambo.
ii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

#### 2.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe amehitimu kidato cha nne, Mtiifu na mwaminifu,awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa na awe Mkazi wa Kata ya Mbalamaziwa.

#### 2.1.2 Malipo

Malipo yatakuwa Tshs.7,000/= kwa siku na malipo hayo yatafanyika mwisho wa mwezi.

## 3.0 WABEBA MAWE (NAFASI 4)

### 3.1 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kubeba mawe yaliyopasuliwa na kuyafikisha kwenye mtambo kwa wakati
ii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

**3.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA**

Awe amehitimu kidato cha nne, Mtiifu na mwaminifu,awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa na awe Mkazi wa Kata ya Mbalamaziwa.

**3.1.2 Malipo**

Malipo yatakuwa Tshs.6,000/= kwa siku na malipo hayo yatafanyika mwisho wa mwezi.

**4.0 MLINZI (NAFASI 3)**

**4.1 KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kulinda eneo zima linalofanyiwa kazi
ii. Kuhakikisha mtambo, na vifaa vingine vyote vinakuwa salama kila wakati
iii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

**4.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA**

Awe amehitimu kidato cha nne, Mtiifu na mwaminifu,awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa na awe Mkazi wa Kata ya Mbalamaziwa. Pia awe amepitia na kufuzu mafunzo ya Jeshi la Akiba au Jeshi la Kujenga Taifa.

**4.1.2 Malipo**

Malipo yatakuwa Tshs.6,000/= kwa siku na malipo hayo yatafanyika mwisho wa mwezi.

**5.0 MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wawe ni raia wa Tanzania, mwananchi wa Kata ya Mbalamaziwa na wenye umri kuanzia miaka 18 usiozidi miaka 35.

ii. Waombaji wote, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa mtendaji wa Kijiji na Kata.

iii. Waombaji wawe na akaunti ya benki (NMB, CRDB au NBC), kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha Mpiga Kura, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) wawili wa kuaminika ambao ni wakazi wa kudumu wa Kata ya Mbalamaziwa.

iv. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

v. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **10/12/2025.**

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na cheti cha kuzaliwa na cheti cha elimu na sifa zingine zilizoainishwa kwenye tangazo hili, Aidha, barua zote za maombi ziletwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi,
S.L.P 223,
**MAFINGA.**

**Tangazo limetolewa na;**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
S.L.P. 223, MAFINGA

Mashaka S. Mfaume
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**